

5	GHARAMA YA UFUNDI (+ Skills Development Levy 4.5% of work service):	TSHS 26,200,000/= SHILINGI MILIONI ISHIRINI NA SITA NA LAKI MBILI TUU.
6	MUDA WA MKATABA (Tangu Kusainiwa kwa Mkataba):	Tarehe ya Kusaini. 28/01/2022 Muda: 90 - SIKU Tarehe ya Kuanza Kazi. 28/01/2022 Tarehe ya Kumaliza Kazi. 27/04/2022
7	MASHARTI YA MALIPO:	<ul style="list-style-type: none"> • Hakuna Malipo ya Awali • Fundi atalipwa kila baada ya sehemu ya kazi husika kukamilika, kukaguliwa na kuthibitishwa.

B: MASHARTI YA JUMLA MKATABA

1. Mwajiri atatoa vifaa vyote vya ujenzi kulingana na maelekezo ya Mtaalamu Mshauri. Zaidi ya hayo mwajiri atatoa maji na umeme.
2. Mwajiri atatoa vitendea kazi vyote kama "concrete mixer", toroli, karai, ndoo, chepe, ngazi, n.k.
3. Fundi atafanya kazi kwa mujibu wa mchanganuo wa kazi na mwongozo wa Mtaalamu Mshauri, kwa umakini na uhodari wa hali ya juu wa kiuafundi.
4. Fundi asipofanya kazi yake vizuri, Mwajiri ana haki ya kumsimamisha kazi na kulipa hasara zote zilitokana na uzembe au makusudi.
5. Fundi atatoa maelekezo ya kazi kwa vibarua wake na mafundi wote aliowaajiri na kuhakikisha kazi inafanywa kulingana na taratibu za kiujenzi.
6. Fundi kwa wakati wote anatakiwa kuhakikisha yeye pamoja na mafundi wake wanazingatia nidhamu na tabia njema na asiajiri kabisa mtu asiyekuwa na utaalumu au ujuzi wa kutosha.
7. Fundi atahusika na vitendo (*kama wizi, uharibifu wa mali za chuo*) vyote vinavyofanywa na mafundi wake na mtu yeoyote anayefanya kazi chini ya usimamizi wake.
8. Fundi kwa wakati wote ahakikishe kuwa eneo la kazi linakuwa safi na salama na pia pindi kazi iishapo ahakikishe vifaa vyote vilivysalia katika eneo la ujenzi kama mabaki vimewekwa sehemu husika na kuacha eneo likiwa safi na salama.
9. Ni marufuku Fundi au mafundi kuja kazini akiwa ametumia aina yoyote ya madawa ya kulevyta, unywaji wa pombe na kuvuta bangi eneo la chuo. Ikibainika atachukuliwa hatua.
10. Mwaajiri hatahusika na malipo yoyote kwa mafundi wasaidizi na vibarua.